

HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO

Mh.mwenyekiti

Kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango,

Halmashauri ya Wilaya ,

URAMBO.

**YAH:TAARIFA YA MGAWO WA FEDHA ZA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA
TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVICO 19**

Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ni miongoni mwa Halmashauri zilizopata mgawo wa fedha Tsh.2,070,000,000.00 ikiwa ni fedha za mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVICO 19.

Fedha hizi ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za Msingi ,sekondari pamoja na idara ya Afya.

Mgawanyo wa fedha hizi ni kama ifuatavyo;

- ✓ Ujenzi wa vyumba 58 vya madarasa kwa Shule za Sekondari Tshs.1,160,000,000.00
- ✓ Ujenzi wa vyumba vya madarasa 22 kwa Shule Shikizi Tshs.440,000,000.00
- ✓ Ujenzi wa jengo la dharura katika Hospitali ya Wilaya ya Urambo Tshs.300,000,000.00
- ✓ Ujenzi wa nyumba ya watumishi watatu katika zahanati ya Itegamatwi Tshs.90,000,000.00
- ✓ Ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalumu Tsh.80,000,000.00

Mh.mwenyekiti ,Mchanganuo wa shule zilizopewa fedha hizi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule shikizi na ujenzi wa madarasa kwa shule za sekondari umeambatanishwa pamoja na taarifa hii.

Aidha kwa upande wa fedha za ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalumu na fedha kwa ajili ya idara ya afya bado hatujapokea mchanganuo wake.

Mh,Mwenyekiti,naomba kuwasilisha.



Baraka M.Zikatimu
Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya
URAMBO